



**Jamhuri ya Muungano wa Tanzania**

**MUHTASARI WA PATO LA TAIFA  
ROBO YA NNE (OKTOBA – DESEMBA), 2019  
MWAKA WA KIZIO 2015**



**Ofisi ya Taifa ya Takwimu  
Wizara ya Fedha na Mipango  
April, 2020**

## **Yaliyomo**

Majedwali .....	2
Viambatisho.....	5
1.0 <i>Utangulizi</i> .....	6
2.0 <i>Matokeo Muhimu</i> .....	6
3.0 <i>Ukuaji wa Uchumi Katika Nchi za Jumuiya ya Afrika Mashariki</i> .....	8
4.0 <i>Ukuaji wa Shughuli za Uchumi</i> .....	9
4.1 <i>Kilimo, Misitu na Uvubi</i> .....	9
4.1.1 <i>Mazao</i> .....	9
4.1.2 <i>Mifugo</i> .....	10
4.1.3 <i>Misitu</i> .....	11
4.1.4 <i>Uvubi</i> .....	11
4.2 <i>Uchimbaji Madini na Mawe</i> .....	11
4.3 <i>Viwanda</i> .....	12
4.4 <i>Umeme</i> .....	12
4.5 <i>Maji Safi na Maji Taka</i> .....	12
4.6 <i>Ujenzi</i> .....	13
4.7 <i>Biashara na Matengenezo</i> .....	14
4.8 <i>Uchukuzi na Uhifadhi wa Mizigo</i> .....	14
4.9 <i>Malazi na Huduma ya Chakula</i> .....	15
4.10 <i>Habari na Mawasiliano</i> .....	15
4.11 <i>Fedha na Bima</i> .....	16
4.12 <i>Upangishaji Majengo</i> .....	16
4.13 <i>Shughuli za Kitalaam, Sayansi na Ufundu</i> .....	17
4.14 <i>Huduma Zinazohusiana na Utawala</i> .....	17
4.15 <i>Utawala na Ulinzi</i> .....	17
4.16 <i>Elimu</i> .....	18
4.17 <i>Afya na Huduma za Jamii</i> .....	18
4.18 <i>Sanaa na Burudani</i> .....	18
4.19 <i>Huduma Nyingine za Kijamii</i> .....	19
4.20 <i>Shughuli za Kaya katika Kuajiri</i> .....	19
5.0 <i>Hitimisho</i> .....	19

## **Majedwali**

Jedwali Na 1: Uzalishaji wa Madini Katika Robo ya Nne Mwaka 2015 – 2019.....	12
--	----



Vielelezo	
Kielelezo 1: Kasi ya Ukuaji wa Pato la Taifa Robo ya Nne, Mwaka 2014 – 2019	7
Kielelezo 2: Mchango wa Shughili Kuu za Kichumi kwa Bei za Miaka Husika	7
Kielelezo 3: Ukuaji wa Pato la Taifa, Robo ya Nne (Oktoba – Desemba) Mwaka 2019	8
Kielelezo 4: Ukuaji wa Uchumi katika Jumuiya ya Afrika Mashariki, Mwaka 2015 – 2019	9
Kielelezo 5: Uzalishaji wa Baadhi ya Mazao, Robo ya Nne Mwaka 2018 na 2019	10
Kielelezo 6: Maji yaliyozalishwa (Mita za Ujazo Milioni), Robo ya Nne, Mwaka 2016 – 2019	13
Kielelezo 7: Thamani ya Mauzo ya Huduma za Mawasiliano, Robo ya Nne Mwaka 2015 – 2019	15
Kielelezo 8: Thamani ya Mikopo na Amana, Oktoba - Desemba, Mwaka 2015 – 2019	16

## **Viambatisho**

Kiambatisho Na.1: Pato la Taifa kwa Shughuli za kiuchumi kwa Bei za Mwaka 2015 – Sh. Milioni .....	20
Kiambatisho Na..2: Ukuaji wa Pato la Taifa kwa Shughuli za Kiuchumi kwa Bei za mwaka 2015 – katika asilimia.....	22
Kiambatisho Na. 3: Pato la Taifa kwa Shughuli za Kiuchumi kwa Bei za Soko (Bei za Miaka inayohusika) – Sh. Milioni .....	24
Kiambatisho Na. 4: Mchango wa Shughuli za Kiuchumi katika Pato la Taifa kwa Bei za Soko (Bei za miaka inayohusika) - katika asilimia .....	26

## **1.0      *Utangulizi***

Muhtasari huu unatoa taarifa za awali za Pato la Taifa kwa bei za miaka husika na bei za mwaka wa kizio wa 2015 kwa Tanzania Bara. Taarifa za Pato la Taifa kwa robo mwaka hutumika kutathmini mabadiliko ya kiuchumi katika vipindi vifupi kwa ajili ya kutayarisha sera za kiuchumi kwa wakati muafaka.


Taarifa zilizotumika kutayarisha takwimu za Pato la Taifa Robo ya nne (Oktoba-Desemba) ya Mwaka 2019 zilikusanywa kutoka katika shughuli zote za uchumi za uzalishaji wa bidhaa na huduma zilizofanyika nchini katika kipindi hicho. Pia, ukokotoaji umezingatia matakwa ya Mfumo wa Umoja wa Mataifa wa Takwimu za Pato la Taifa unaojulikana kama ***System of National Accounts 2008***.

Vile vile, Ofisi ya Taifa ya Takwimu inatekeleza sera ya marekebisho ya takwimu za Pato la Taifa ambayo ilianza kutumika mwanzoni mwa mwaka 2019. Sera hii inaruhusu kuchapisha matokeo ambayo yanaweza kufanyiwa marekebisho kulingana na upatikanaji wa takwimu mpya za kila robo mwaka na za kila mwaka.

## **2.0      *Matokeo Muhimu***


Katika kipindi cha robo ya nne (Oktoba - Desemba) ya mwaka 2019, Pato la Taifa kwa bei za miaka husika lilikuwa na thamani ya shilingi trilioni 39.1 ikilinganishwa na shilingi trilioni 34.5 katika robo ya nne ya mwaka 2018. Vile vile, thamani ya Pato la Taifa kwa bei za mwaka wa kizio wa 2015 iliongezeka hadi shilingi trilioni 33.7 katika robo ya nne ya mwaka 2019 kutoka shilingi trilioni 31.5 katika robo ya nne ya mwaka 2018, sawa na ukuaji wa asilimia 7.0.

**Kielelezo 1: Kasi ya Ukuaji wa Pato la Taifa Robo ya Nne, Mwaka 2014 – 2019**




Mchango wa shughuli za uchumi kwa kuzingatia mchanganuo wa shughuli kuu za kiuchumi za msingi (*primary activities*), shughuli za kati (*secondary activities*) na shughuli za huduma (*tertiary activities*) unaonesha kuwa shughuli za Msingi zilichangia asilimia 37.7 zikifuatiwa na shughuli za Huduma asilimia 37.5 na shughuli za Kati asilimia 24.8. Mchango huu umekokotolewa kabla ya kujumuisha kodi katika bidhaa na huduma.

**Kielelezo 2: Mchango wa Shughili Kuu za Kichumi kwa Bei za Miaka Husika**



Shughuli ya Uchimbaji Madini na Mawe ilikuwa na kasi ya kubwa ya ukuaji wa asilimia 21.5 ikifuatiwa na Sanaa na Burudani asilimia 13.9, wakati Ujenzi na Habari na Mawasiliano ziliongezeka kwa asilimia 11.0.


**Kielelezo 3: Ukuaji wa Pato la Taifa, Robo ya Nne (Oktoba – Desemba) Mwaka 2019**



### **3.0      *Ukuaji wa Uchumi Katika Nchi za Jumuiya ya Afrika Mashariki***

Ukuaji wa uchumi mionganoni mwa nchi wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki katika kipindi cha robo ya nne mwaka 2019 ulioneshwa kuwa: Uchumi wa Rwanda uliongezeka kwa asilimia 8.4 ikilinganishwa na asilimia 9.6 mwaka 2018. Uchumi wa Uganda uliongezeka kwa asilimia 3.6 ikilinganishwa na ukuaji wa asilimia 7.5 mwaka 2018 wakati uchumi wa Tanzania uliongezeka kwa asilimia 7.0 mwaka 2019 ikilinganishwa na asilimia 7.1 mwaka 2018. Taarifa za ukuaji wa uchumi kwa nchi za Kenya, Burundi na Sudani Kusini bado hazijatolewa.

**Kielelezo 4: Ukuaji wa Uchumi katika Jumuiya ya Afrika Mashariki, Mwaka 2015 – 2019**



#### **4.0      *Ukuaji wa Shughuli za Uchumi***

Shughuli za kiuchumi zilizochangia katika ukuaji wa uchumi kwa asilimia 7.0 katika robo ya nne ya mwaka 2019 ni pamoja na kilimo; uchimbaji madini na mawe; uzalishaji viwandani; umeme na maji; ujenzi; biashara na uchukuzi na uhifadhi wa mizigo. Shughuli nyingine ni habari na mawasiliano; fedha na Bima; Utawala na Ulinzi, Elimu na Afya. Maelezo ya kina kwa baadhi ya shughuli za kiuchumi ni kama ifuatavyo:

##### **4.1    *Kilimo, Misitu na Uvuvi***

Shughuli hii inahusika na uvunaji wa rasilimali za asili za mboga mboga za majani na za wanyama zinazojumuisha mazao ya kupandwa, ufugaji na uzalishaji wa wanyama, uvunaji wa miti na mimea mingine, wanyama au bidhaa za wanyama kutoka katika mashamba ya ufugaji au mazingira ya asili.


###### **4.1.1 *Mazao***

Mazao makuu yaliyohusishwa ni pamoja na mahindi, mpunga, ulezzi/mtama, nafaka nyingine, Mihogo, viazi mviringo, viazi vitamu, maharagwe, mikunde, mbegu za mafuta, mboga mboga, ndizi, matunda mengine, karanga, kahawa, pamba, chai, tumbaku na mazao mengine ya chakula na biashara.

Shughuli ya uzalishaji wa mazao iliongezeka kwa kiwango cha asilimia 6.1 katika robo ya nne ya mwaka 2019 ikilinganishwa na asilimia 2.9 katika kipindi kama hicho

mwaka 2018. Ukuaji wa shughuli ya mazao ulitokana na upatikanaji wa mvua za kutosha katika maeneo ya uzalishaji wakati wa msimu wa mvua za vuli.

**Kielelezo 5: Uzalishaji wa Baadhi ya Mazao, Robo ya Nne Mwaka 2018 na 2019**



Mazao ambayo yalichangia kwa kiasi kikubwa katika ukuaji wa shughuli ya mazao katika robo ya nne ya mwaka 2019 ni pamoja na mahindi ambayo yaliongezeka kwa asilimia 2.1 kutoka tani elfu 3,191 mwaka 2018 hadi tani elfu 3,260 mwaka 2019. Viazi vitamu viliongezeka kwa asilimia 5.7 kutoka tani elfu 131 mwaka 2018 hadi tani elfu 139 mwaka 2019. Maharage na mazao jamii ya mikunde yaliongezeka kwa asilimia 3.7 kutoka tani elfu 354 mwaka 2018 hadi tani elfu 367 mwaka 2019. Viazi mviringo viliongezeka kwa asilimia 60 kutoka tani elfu 17 mwaka 2018 hadi tani elfu 27 mwaka 2018. Mpunga uliongezeka kwa asilimia 10.1 kutoka tani elfu 590 mwaka 2018 hadi tani elfu 650 mwaka 2019.

#### **4.1.2 *Mifugo***

Shughuli hii inahusika na ufugaji ng'ombe wa asili na wa kisasa, mbuzi; kondoo; punda, farasi; nguruwe, sungura, kuku wa kienyeji na kisasa; na ndege wa aina nyigine.

Shughuli ya mifugo iliongezeka kwa kiwango cha asilimia 4.9 katika robo ya nne ya mwaka 2019 kiwango ambacho ni sawa na ilivyokuwa katika kipindi kama hicho mwaka 2018. Kiwango cha ukuaji kilitokana na kuongezeka kwa mahitaji ya bidhaa za mifugo ambazo ziliongezeka kwa kiasi kikubwa kutokana na kuongezeka kwa pato

la wastani la mwananchi, kupanuka kwa miji, pamoja na kuongezeka kwa uelewa wa wananchi kuhusu lishe bora.

#### **4.1.3 Misitu**

Shughuli hii inahusisha uzalishaji na uvunaji wa mazao ya misitu kama vile magogo, mkaa, kuni, matawi ya mtii, na bidhaa nyingine zisizo za miti.

Shughuli ya uzalishaji wa misitu ilikua kwa kiwango cha asilimia 6.4 katika robo ya nne ya mwaka 2019 ikilinganishwa na asilimia 5.2 katika kipindi kama hicho mwaka 2018. Ukuaji huo ulitokana na kuongezeka kwa usimamizi wa rasilimali za misitu na pia juhudii za Serikali kuhakikisha uvunaji endelevu ya bidhaa za misitu.

#### **4.1.4 Uvuvi**

Shughuli ya uvuvi inahusika na uvunaji wa rasilimali za uvuvi katika maji ya bahari na vyanzo vingine vya maji baridi.

Shughuli hii ilikua kwa kiwango cha asilimia hasi 8.8 katika robo ya nne ya mwaka 2019 ikilinganishwa na asilimia 15.4 katika robo ya nne ya mwaka 2018. Kiwango cha ukuaji kilitokana na kupungua kwa samaki na mazao ya samaki yaliyovunwa katika kipindi hicho.

### **4.2 Uchimbaji Madini na Mawe**

Shughuli ya madini na mawe inahusisha uchimbaji wa madini yabisi kama vile makaa ya mawe, aina ya vimiminika (petroli) au gesi (gesi asilia). Uchimbaji hufanyika chiniya ardhi, ukusanyaji juu ya ardhi au kwenye visima. Pia unajumuisha shughuli za ziada zinazolenga kutayarisha madini kwa ajili ya kuuzwa, kwa mfano, kusaga, kusafisha na kukausha. Shughuli hizi mara nyingi zinafanywa na vitengo ambavyo vinavuna rasilimali za madini / au nyingine zilizopo karibu na migodi.

Shughuli ya uchimbaji wa madini na mawe iliongezeka kwa kiwango cha asilimia 21.5 katika robo ya nne ya mwaka 2019 ikilinganishwa na asilimia 3.2 katika kipindi kama hicho mwaka 2018. Ukuaji ulitokana na kuongezeka kwa kiasi cha madini ya dhahabu, fedha na gesi asilia yaliyovunwa. katika kipindi cha robo ya nne ya mwaka 2019. Uzalishaji wa dhahabu uliongezeka hadi kilo 15,216 katika robo ya nne mwaka 2019 kutoka kilo 10,966 kipindi kama hicho mwaka 2018. Uzalishaji wa madini ya fedha uliongezeka hadi kilo 3,717 kutoka tani 3,237 katika kipindi kama hicho mwaka 2018, Uzalishaji wa Makaa ya mawe uliongezeka kwa asilimia 35 hadi kufikia tani

194,151 mwaka 2019 ikilinganisha na tani 144,171 mwaka 2018 wakati gesi asilimia iliongezeka hadi futi za ujazo milioni 16,760 mwaka 2019 kutoka futi za ujazo milioni 15,872 mwaka 2018.

**Jedwali Na 1: Uzalishaji wa Madini Katika Robo ya Nne Mwaka 2015 – 2019**

Madini	Kipimo	2015	2016	2017	2018	2019
Makaa ya Mawe	Tani	75,426	104,010	163,836	144,171	194,151
Dhahabu	Kilo	14,311	11,389	11,737	10,966	15,216
Madini ya Fedha	Kilo	4,605	4,615	2,656	3,237	3,717
Gesi asilia	Mscf	12,305	12,257	13,075	15,872	16,760

#### **4.3 Viwanda**

Shughuli ya uzalishaji viwandani inahusisha ubadilishaji au uchakataji wa bidhaa katika hali yake kawaida na kuzalisha bidhaa za aina nyingine ambazo zinaweza kutumika moja kwa moja na mlaji wa mwisho au kutumika kuzalisha bidhaa nyingine. Bidhaa zinazoweza kuchakatwa ni pamoja na bidhaa za kilimo, misitu, uvuvi, madini na bidhaa nyingine za viwanda.

Shughuli ya uzalishaji viwandani iliongezeka kwa kasi ya asilimia 4.7 katika robo ya nne ya mwaka 2019 ikilinganishwa na asilimia 16.7 katika robo ya nne mwaka 2018. Kiwango cha ukuaji kilitokana na kuongezeka kidogo kwa uzalishaji wa bidhaa za viwandani kwa jumla.

#### **4.4 Umeme**

Shughuli hii inahusika na uzalishaji na usambazaji wa umeme na gesi asilia, kupitia miundombinu ya kudumu ya waya na mabomba. Uzalishaji wa umeme ni kutoka katika vyanzo vya maji, mafuta na gesi. Pia inahusika na shughuli za usambazaji na ugawaji wa umeme. Vyanzo vya vikuu vya takwimu za uzalishaji umeme ni kutoka katika makampuni ya uzalishaji wa umeme.

Katika kipindi hicho shughuli hiyo iliongezeka kwa kiwango cha asilimia 2.0 ikilinganishwa na ukuaji wa asilimia 9.8 katika robo ya nne ya mwaka 2018.

#### **4.5 Maji Safi na Maji Taka**


Shughuli hii inahusika na kukusanya na kusafisha maji kwa ajili ya ugavi wa maji, kusafisha maji ya bahari kwa kuondoa chumvi ili kuweza kuzalisha maji ya kutumia kama bidhaa kuu na kukusanya maji moja kwa moja kutoka katika visima kwa ajili ya

matumizi ya makampuni ya maji au matumizi binafsi katika kilimo au kaya. Pia inajumuisha shughuli za usambazaji wa maji.

Ukuaji wa shughuli ya maji inategemea wingi wa maji yaliyozosalishwa. Katika kipindi cha Oktoba hadi Desemba 2019, kiasi cha maji kilichozosalishwa kiliongezeka hadi mita za ujazo milioni 87.9 kutoka mita za ujazo milioni 85.3 zilizozosalishwa katika robo ya nne mwaka 2018.

Katika kipindi hicho, shughuli hii iliongezeka kwa kiwango cha asilimia 2.9 ikilinganishwa na asilimia 8.3 katika robo ya nne ya mwaka 2018. Ukuaji wa shughuli hii ilitokana na kuboreshwa kwa miundombinu ya uzalishaji wa maji na kuongezeka kwa uwezo wa mitambo ya uzalishaji maji na pia ongezeko la mahitaji ya maji kutokana na kuongezeka kwa idadi ya watu hasa katika maeneo ya mijini iliyochochea uzalishaji wa maji ili kuendana na mahitaji.

**Kielelezo 6: Maji yaliyozosalishwa (Mita za Ujazo Milioni), Robo ya Nne, Mwaka 2016 – 2019**



#### **4.6 Ujenzi**

Shughuli hii inajumuisha ujenzi wa jumla na shughuli maalumu za ujenzi kwa ajili ya majengo na kazi za uhandisi. Inajumuisha pia ujenzi mpya, ukarabati, kufanya mabadiliko makubwa kwenye majengo, na ujenzi wa miundombinu.

Ujenzi wa jumla ni ujenzi wa nyumba nzima, majengo ya biashara/ofisi, maduka na majengo mengine ya umma na miundombinu ya mashambani. Ujenzi pia unajumuisha

ujenzi wa barabara, madaraja, reli, viwanja vya ndege, bandari na miundombinu ya maji, mifumo ya umwagiliaji, mifumo ya maji taka, miundombinu ya viwanda, mabomba na mifumo ya umeme na vituo vya michezo.

Shughuli ya ujenzi iliongezeka kwa kiwango cha asilimia 11.0 katika robo ya nne ya mwaka 2019, ikilinganishwa na asilimia 17.3 katika robo ya nne ya mwaka 2018. Ukuaji ulitokana na kuongezeka kwa uzalishaji wa ndani wa vifaa vya ujenzi kama saruji, chuma na vyuma ambavyo ni viashiria vinavotumika kutathmini ukuaji wa shughuli ya ujenzi.

#### ***4.7 Biashara na Matengenezo***

Shughuli hii inajumuisha uuzaji wa jumla na uuzaji wa rejareja (uuzaji wa bidhaa bila ya kufanya mabadiliko) wa aina yoyote ya bidhaa, pamoja na utoaji wa huduma kwa ajili ya uuzaji wa bidhaa. Pia inahusisha ukarabati wa magari na usimikaji na ukarabati wa bidhaa za binafsi na za nyumbani. Shughuli kuu ni kununua na kuuza bidhaa.

Shughuli ya uuzaji wa bidhaa wa jumla na rejareja iliongezeka kwa kasi ya asilimia 5.2 katika robo ya nne ya mwaka 2019 ikilinganishwa na kiwango cha ukuaji wa asilimia 8.0 katika robo ya nne ya mwaka 2018. Ukuaji huo ulitokana na kuongezeka kwa bidhaa za biashara hususan bidhaa za kilimo na bidhaa zilizoagizwa kutoka nje ya nchi.

#### ***4.8 Uchukuzi na Uhifadhi wa Mizigo***

Shughuli hii inahusisha utoaji wa huduma ya usafiri wa abiria au/na mizigo, ikiwa ni kwa ratiba maalum au isiyokuwa na ratiba, kwa njia ya reli, bomba, barabara, maji au anga na shughuli zinazohusiana ikiwa ni pamoja na utunzaji wa mizigo na uhifadhi. Shughuli hii pia inajumuisha kukodisha vifaa vya usafiri na madereva na shughuli za posta na usafirishaji wa vifurushi.

Shughuli ya usafirishaji na uhifadhi wa mizigo iliongezeka kwa kiwango cha asilimia 8.4 katika robo ya nne ya mwaka 2019 ikilinganishwa na asilimia 12.6 katika kipindi kama hicho mwaka 2018. Kiwango cha ukuaji kilitokana na kuongezeka kwa idadi ya abiria na mizigo iliyosafirishwa katika kipindi hicho.

#### **4.9 Malazi na Huduma ya Chakula**


Shughuli hii inajumuisha utoaji huduma ya makazi ya muda mfupi kwa wageni na wasafiri wengine na utoaji wa huduma ya chakula na vinywaji kwa mlaji wa mwisho. Huduma ya malazi na chakula ilikua kwa kiwango cha asilimia 3.9 katika robo ya nne ya mwaka 2019 ikilinganishwa na kiwango cha asilimia 1.9 mwaka 2018. Kasi ya ukuaji ilitokana na ongezeko la watalii pamoja na ongezeko la vitanda viliviyotumika kulala wageni katika kipindi hicho. Katika kipindi hicho, idadi ya watalii walikuwa 418,227 ikilinganishwa na watalii 375,132 katika robo ya nne ya mwaka 2018.

#### **4.10 Habari na Mawasiliano**

Shughuli hii inahusika na uchapishaji, upigaji wa picha za kawaida, picha za video na uzalishaji wa programu za televisheni, kurekodi sauti na kuchapisha muziki, shughuli za programu na utangazaji, kwa mfano, utangazaji wa radio na televisheni, mawasiliano ya simu, programu za kompyuta, ushauri na shughuli zinazohusiana na shughuli za huduma za habari kama vile uchakataji wa data.

Shughuli hii imekua kwa kiwango cha asilimia 11.0 katika robo ya nne ya mwaka 2019 ikilinganishwa na asilimia 4.4 katika robo ya nne ya mwaka 2018. Kiwango cha ukuaji kilitokana na kuongezeka kwa muda wa maongezi uliotumiwa na wateja wa simu za mkononi na upanuzi wa huduma za utangazaji na mtandao.

**Kielelezo 7: Thamani ya Mauzo ya Huduma za Mawasiliano, Robo ya Nne Mwaka 2015 – 2019**




#### **4.11 Fedha na Bima**

Shughuli hii inahusika na utoaji wa huduma za fedha, bima, pensheni ya hiari, na huduma nyingine za fedha.

Shughuli ya fedha na bima ilikua kwa kiwango cha asilimia 3.8 katika robo ya nne ya mwaka 2019 ikilinganishwa na ukuaji wa asilimia hasi 0.5 katika robo ya nne ya mwaka 2018. Ukuaji wa shughuli hii ultokana na kuongezeka kwa amana kwa asilimia 5.9 kutoka shilingi trilioni 20.6 katika robo ya nne ya mwaka 2018 hadi shilingi trilioni 21.8 katika robo ya nne ya mwaka 2019. Vile vile, mikopo iliongezeka kwa asilimia 11.3 kutoka shilingi trilioni 17.1 katika robo ya nne ya mwaka 2018 hadi shilingi trilioni 19.1 katika robo ya nne ya mwaka 2019; na pia kuongezeka kwa huduma zinazotolewa na makampuni ya bima.

**Kielelezo 8: Thamani ya Mikopo na Amana, Oktoba - Desemba, Mwaka 2015 – 2019**



#### **4.12 Upangishaji Majengo**

Shughuli hii inahusika na utoaji wa huduma za kuuza au kununua majengo, kukodisha mali, majengo na pia kutoa huduma nyingine za mali isiyohamishika ikiwa ni pamoja na kupima mali isiyohamishika.

Kiwango cha ukuaji katika kipindi cha Oktoba hadi Desemba mwaka 2019 kilikuwa asilimia 4.5 ambacho kilikuwasawa na kiwango cha ukuaji katika kipindi kama hicho mwaka 2018. Ukuaji wa shughuli hii ultokana na kuongezeka kwa mahitaji ya nyumba za kuishi na biashara hususan katika maeneo ya mijini.

#### **4.13 Shughuli za Kitalaam, Sayansi na Ufundi**

Shughuli hii inajumuisha shughuli maalumu za kitalaam, kisayansi na kiufundi. Shughuli hizi zinahitaji kiwango cha juu cha mafunzo, pamoja na kupata ujuzi maalum unaotumika kutoa huduma kwa watumiaji.

Shughuli hii inahusisha huduma za kisheria na uhasibu; ushauri na usimamizi; usanifu na uhandisi; kupima na uchambuzi wa kitaalamu; utafiti wa kisayansi na maendeleo; matangazo na utafiti wa masoko; utaalamu wa aina nyingine wa kisayansi na kiufundi pamoja na shughuli za ugani.

Shughuli hii iliongezeka kwa kiwango cha asilimia 9.3 katika robo ya nne ya mwaka 2019 ikilinganishwa na asilimia 6.9 katika robo ya nne ya mwaka 2018. Kiwango cha ukuaji kilitokana na kuongezeka kwa mahitaji ya shughuli za kitaaluma, kisheria na kiuhasibu.

#### **4.14 Huduma Zinazohusiana na Utawala**

Shughuli hii inajumuisha huduma zinazosaidia biashara kufanyika. Shughuli inajumuisha huduma za kukodisha vifaa, ajira, huduma za uwakala wa mashirika ya usafiri, huduma za kuongoza watalii, huduma za kuandaa malazi; na huduma nyingine zinazohusiana na usalama na uchunguzi; pamoja na huduma kwenye majengo na uboreshaji wa mazingira.

Kiwango cha ukuaji kiliongezeka kwa asilimia 8.2 katika robo ya nne ya mwaka 2019 ikilinganishwa na asilimia 6.1 katika robo ya nne ya mwaka 2018. Kiwango cha ukuaji kilitokana na kuongezeka kwa huduma za wakala wa usafiri wa abiria na shughuli za makapuni ya kuongoza watalii.

#### **4.15 Utawala na Ulinzi**

Shughuli ya utawala na ulinzi pamoja na majukumu mengine inahusika na kutunga na kutafisiri sheria, kukusanya kodi, ulinzi, usalama wa raia na mali zao, huduma za uhamiaji, na uendeshaji wa serikali kwa ujumla. Vile vile, mifuko ya lazima (compulsory) ya hifadhi ya jamii inajumuishwa katika shughuli hii.

Kiwango cha ukuaji wa shughuli hii kilikuwa asilimia 4.5 katika robo ya nne ya mwaka 2019 ikilinganishwa na asilimia 1.8 katika robo ya nne ya mwaka 2018.

Ukuaji ulitokana na kuongezeka kwa matumizi ya Serikali katika kutoa huduma za utawala na ulinzi.

#### ***4.16 Elimu***

Shughuli hii inajumuisha utoaji wa elimu katika ngazi yoyote, kwa njia ya kuongea au maandishi au kwa njia ya redio na televisheni au njia nyingine za mawasiliano. Inajumuisha elimu inayotolewa na taasisi tofauti katika mfumo wa kawaida wa shule katika ngazi tofauti tofauti pamoja na elimu ya watu wazima na elimu ya kujifunza kusoma na kuandika. Shughuli hii inajumuisha elimu katika sekta ya umma na binafsi. Shughuli hii ilikua kwa kiwango cha asilimia 5.2 katika robo ya nne ya mwaka 2019 ikilinganishwa na asilimia 5.0 katika robo ya nne ya mwaka 2018. Ukuaji ulitokana na kuongezeka kwa idadi ya wanafunzi waliodahiliwa katika shule za msingi na sekondari pamoja na ongezeko la matumizi ya serikali katika utoaji wa huduma za elimu.

#### ***4.17 Afya na Huduma za Jamii***

Shughuli hii inajumuisha utoaji wa huduma za afya na maendeleo ya jamii. Inajumuisha huduma za afya zinazotolewa na wataalam wa matibabu walioelimishwa katika hospitali na vituo vingine, shughuli nyingine za huduma za makazi ambazo zinahusisha shughuli za huduma za afya kwa jamii bila ushirikishwaji wa wataalamu wa huduma za afya.

Shughuli hii ilikua kwa kiwango cha asilimia 6.8 katika robo ya nne ya mwaka 2019 ikilinganishwa na asilimia 2.2 katika robo ya nne ya mwaka 2018. Kiwango cha ukuaji kilitokana na kuongezeka kwa idadi ya wagonjwa waliohudumiwa katika vituo vya afya vya umma na vya binafsi.

#### ***4.18 Sanaa na Burudani***

Shughuli hii inajumuisha shughuli mbalimbali zinazotolewa ili kukidhi maslahi mbalimbali ya kitamaduni, na utoaji wa burudani kwa umma kwa ujumla. Shughuli hii pia inahusika na burudani za bendi, uendeshaji wa maeneo ya makumbusho, kamari, shughuli za huduma michezo na burudani kwa ujumla.

Kiwango cha ukuaji kiliongezeka kwa asilimia 13.9 katika robo ya nne ya mwaka 2019 ikilinganishwa na asilimia 9.8 katika robo ya nne ya mwaka 2018. Ukuaji ulitokana na kuongezeka kwa mauzo ya bidhaa za kitamaduni kwa watalii waliotembelea vivutio mbalimbali katika kipindi husika.

#### ***4.19 Huduma Nyingine za Kijamii***

Shughuli hii inajumuisha shughuli za mashirika ya uanachama, ukarabati wa vifaa vya kieletroniki na bidhaa za kibinafsi za nyumbani na shughuli mbalimbali za huduma za binafsi ambazo hazijajumuishwa kwenye shughuli nyingine kwenye mwongozo wa kuainisha shughuli za kiuchumi.

Shughuli hii iliongezeka kwa kiwango cha asilimia 8.1 katika robo ya nne ya mwaka 2019 ikilinganishwa na asilimia 4.7 katika robo ya nne ya mwaka 2018. Kiwango cha ukuaji kilitokana na ongezeko la idadi ya wananchi wanaoishi katika maeneo ya mijini na shughuli za kibinafsi.

#### ***4.20 Shughuli za Kaya katika Kuajiri***

Shughuli za kaya kama mwajiri zinajumuisha wafanyakazi wa ndani kama vile wajakazi, wapishi, wahudumu, wafugaji, watengenezaji wa bustani, wakulima, walini wa mlangoni, waendeshaji wa gari, waangalizi wa Watoto, wafundishaji na masekretari. Bidhaa na huduma zinazozalishwa na shughuli hii hutumiwa na kaya inayoajiri.

Shughuli hii iliongezeka kwa kasi ya asilimia 3.1 katika robo ya nne ya mwaka 2019 sawa na ilivyokuwa katika kipindi kama hicho mwaka 2018. Kiwango cha ukuaji kilitokana na ongezeko la wakazi wa mijini.

### ***5.0 Hitimisho***

Pato la Taifa kwa robo mwaka hupima shughuli za kiuchumi katika vipindi vifupi vifupi. Kasi ya ukuaji wa uchumi katika kipindi cha robo ya nne (Oktoba – Desemba) mwaka 2019 iliongezeka kwa asilimia 7.0 ikilinganishwa na asilimia 7.1 katika kipindi kama hicho mwaka 2018. Katika kipindi hicho, shughuli ya Uchimbaji Madini na Mawe iliongezeka kwa kasi kubwa ya ukuaji wa asilimia 21.5 ikifuatiwa na Sanaa na Burudani asilimia 13.9 na Ujenzi na Habari na Mawasiliano ziliongezeka kwa asilimia 11.0.

**Kiambatisho Na.1: Pato la Taifa kwa Shughuli za kiuchumi kwa Bei za Mwaka 2015 – Sh. Milioni**

Mwaka	Robo mwaka	kilimo	Madini na Mawe	Viwanda	Umeme	Maji safi na maji taka	Ujenzi	Biashara na Matengenezo	Malazi na Huduma ya Chakula	Uchukuzi na Uhifadhi Mizigo	Habari na Mawasiliano	Fedha na Bima
2012		21,807,030	3,314,742	6,066,989	669,069	358,361	7,578,263	7,371,411	1,343,924	5,710,466	1,266,747	3,444,161
2013		22,408,192	3,464,721	6,292,514	723,608	367,890	9,023,353	7,682,286	1,356,204	6,050,976	1,414,116	3,405,940
2014		23,952,077	3,687,273	6,919,794	815,297	381,760	9,253,082	8,444,243	1,397,782	6,577,706	1,560,064	3,764,113
2015		25,234,560	4,055,619	7,411,672	798,801	390,758	10,446,797	8,747,862	1,421,916	6,929,895	1,681,098	4,189,021
2016		26,436,338	4,356,709	8,213,364	869,262	417,899	11,960,720	9,260,703	1,480,052	7,324,856	1,718,548	4,235,515
2017		28,008,976	4,588,624	8,889,818	877,667	444,660	13,765,005	9,821,248	1,525,619	7,815,845	1,824,471	4,115,393
2018		29,482,834	4,659,195	9,623,501	928,174	477,510	15,546,664	10,395,783	1,604,391	8,736,561	1,989,829	4,094,972
2012	1	5,972,854	845,470	1,528,195	151,473	86,422	1,816,993	1,877,418	321,003	1,208,445	281,981	849,590
	2	5,182,996	825,383	1,544,666	164,427	89,319	1,808,760	1,855,404	320,427	1,456,176	303,507	844,631
	3	4,092,001	833,592	1,499,895	172,946	92,526	2,012,312	1,725,714	358,248	1,489,645	327,526	886,247
	4	6,559,178	810,297	1,494,233	180,223	90,094	1,940,197	1,912,875	344,245	1,556,199	353,733	863,692
2013	1	5,994,220	748,412	1,459,422	167,460	87,306	2,146,785	1,828,162	332,454	1,519,508	312,238	811,387
	2	5,376,452	850,463	1,547,040	177,004	90,069	2,111,891	1,884,307	324,659	1,501,581	343,060	836,571
	3	4,199,755	875,290	1,677,731	181,477	85,918	2,389,873	1,893,295	354,104	1,513,039	358,452	881,698
	4	6,837,765	990,556	1,608,322	197,667	104,598	2,374,804	2,076,522	344,987	1,516,849	400,366	876,284
2014	1	6,335,448	937,448	1,621,405	201,849	87,893	2,182,230	2,054,479	346,623	1,625,429	342,909	912,095
	2	5,877,120	871,899	1,706,772	182,845	94,708	2,507,336	2,073,942	339,327	1,616,710	380,305	927,895
	3	4,450,294	929,381	1,788,128	213,998	97,099	2,228,708	2,035,245	361,470	1,686,150	414,058	960,721
	4	7,289,215	948,546	1,803,489	216,605	102,059	2,334,808	2,280,578	350,362	1,649,417	422,793	963,401
2015	1	6,605,887	923,326	1,733,636	211,828	96,862	2,438,046	2,093,973	346,778	1,654,599	386,446	995,846
	2	6,347,239	965,335	1,820,111	199,281	92,862	2,690,105	2,195,254	345,054	1,676,064	412,841	1,011,653
	3	4,656,388	960,427	1,939,664	192,215	99,585	2,601,253	2,162,776	372,080	1,764,202	441,478	1,076,143
